

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI - TABORA



S.L.P. 62, TABORA, TANZANIA

Simu: +255 (0) 26 2605058

Nukushi: +255 (0) 26 2605338

BaruaPepe: info@bti.ac.tz

Tovuti: www.bti.ac.tz

Kumb. Na. B/TRA/I/VOL. IV/10

09/05/2018

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA KOZI ZA UFUGAJI NYUKI KWA MWAKA WA
MASOMO 2018/2019**

Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora kinatangaza nafasi za masomo kwa mwaka wa masomo 2018/2019 katika ngazi ya Stashahada na Astashahada.

Kozi zinazotangazwa

- i. Astashahada ya Ufugaji Nyuki: Miaka miwili (2) (NTA - Level 5)
- ii. Stashahada ya Ufugaji Nyuki: Miaka miwili (2) (NTA – Level 6)

A. Sifa za Mwombaji:

Kozi ya Astashahada (Technician Certificate) ya Ufugaji Nyuki

- i. Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne na awe amefaulu na kupata angalau alama D zisizopungua nne (4), kati ya hizo lazima awe amefaulu mojawapo ya masomo yafuatayo: Biolojia au Kemia au Fizikia au Jiografia au Sayansi Kilimo.

AU

Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya VETA ngazi ya tatu (NVA Level III) katika taaluma ya ufugaji nyuki kutoka kwenye chuo kinachotambulika na awe amemaliza kidato cha nne

Kozi ya Stashahada (Ordinary Diploma) ya Ufugaji Nyuki

- i. Awe amemaliza kidato cha sita na awe amefaulu na kupata angalau alama E isiyopungua moja na S moja katika masomo ya Hisabati, Biolojia, Kemia, Jiografia, Fizikia na Sayansi Kilimo.

AU

Mwombaji awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya Astashahada (**Technician Certificate**) katika fani ya Ufugaji Nyuki, Misitu, Wanyamapori, Kilimo au Mafunzo ya Astashahada yanayolandana na taaluma ya ufugaji nyuki kutoka kwenye chuo kinachotambulika.

B. Ada

Waombaji watakoachaguliwa watatakiwa kulipa ada kama ifuatavyo:

- i. Mwaka wa kwanza: **Astashahada na Stashahada** Sh 805,000/= AU Dola za Kimarekani (USD) 1,380.00 kwa waombaji wasio na uraia wa Tanzania.
- ii. Mwaka wa pili: **Astashahada na Stashahada** Sh 775,000/= AU Dola za Kimarekani (USD) 1,250.00 kwa waombaji wasio na uraia wa Tanzania.

Muhimu:

- a. Ada yaweza kulipwa yote kwa awamu moja mwanzo wa mwaka wa masomo au kwa awamu mbili – nusu mwanzo wa muhula wa kwanza na nusu nyingine mwanzo wa muhula wa pili.
- b. Ada hiyo haihusishi gharama za chakula, malazi, mafunzo kwa vitendo (field attachment) na mavazi ya kinga.
- c. Nafasi chache za hosteli zinapatikana chuoni kwa gharama ya Sh 270,000/= kwa mwaka inayolipwa kwa awamu moja au mbili.

ANGALIZO: Ada zinaweza kubadilika wakati wowote ndani ya kipindi cha mafunzo kadiri itakavyoonekana ni muhimu.

C. Jinsi ya Kutuma maombi

- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo gharama yake ni **Sh 10,000/=**
- Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi vya taaluma pamoja na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay –in Slip) kwa ajili ya fomu.
- Fomu za maombi zinapatikana Chuoni na kwenye Tovuti ya Chuo; <http://www.bti.ac.tz>

NB. Waombaji wote wanapaswa kutambua kuwa kwa sasa udahili utafanyika chuoni, hivyo waombaji wote wanapaswa kutuma maombi chuoni.

D. Mwisho wa kutuma maombi

Mwisho wa kutuma maombi ni Tarehe **24 Agosti 2018**. Aidha, maombi yatakayotumwa baada ya Tarehe iliyotajwa hayatafanyiwa kazi.

Maombi yote yatumwe kwa:

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki,
S.L.P 62,
TABORA.
Barua pepe: info@bti.ac.tz

E. Taarifa kwa watakaochaguliwa.

Majina ya watakaochaguliwa yatatangazwa kwenye tovuti ya Chuo (www.bti.ac.tz) na kwenye mbao za matangazo za Chuo.

Tangazo hili limetolewa na:

Mkuu wa Chuo, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki
Kny: Katibu Mkuu

Wizara ya Maliasili na Utalii